



WEST SHORE  
SCHOOL DISTRICT

# Welcome Handbook

**SWAHILI**





# Karibu

## **katika shule ya Wilayani West Shore**

Wazazi na shule hufanya kazi pamoja kwa masomo ya watoto. Wote hutaka watoto wafanye vyema shuleni. Wazazi na familia wakija pamoja kuwasaidia masomoni, watoto wao hufanya vyema na kunawili kimaisha.

Njia moja ya kufanya kazi pamoja ni kwa wazazi na walimu kusemezana. Tunaweza kupata watafsiri na wakalimani wa kukusaidia. Kama unataka kuongea na mfanyakazi yeyote ofisini na huongi kwa lugha ya kingereza, unaweza piga simu shuleni na useme jina la mwanao, ujitambulisha kama (mamake, babake, mlezi), lugha unayoelewa na namba yako ya simu. Pia unaweza andika maelezo hayo na utume shuleni. Mfanyakazi wa shule atakupia simu na mkalimani haraka iwezekanavyo.

Tunakuhamasisha usome maelezo muhimu kuhusu shule yetu kwenye hiki kitabu. Kama una maswali yoyote, tafadhali piga simu shuleni kwa maelezo zaidi.

*Hiki kitabu kilichapishwa mwaka wa 2009-2010 na kusahihishwa mwaka wa 2022 na fedha za mada III*

## Mahudhurio

Ni nini kitakackofanyika kama mwanangu hatakwenda shuleni?

Sheria za shule hapa Pennsylvania zahitaji kila mwanafunzi wa umri wa miaka sita(6) hadi 18 ahudhuri shule. Ni muhimu kwa kila mwanafunzi kuja shuleni kila siku.

Mwanafunzi anaweza kukosa kuja shuleni kwa sababu zifuatazo:

- Magonjwa
- Kifo cha mtu wa familia wa karibu
- Sababu ya dharura ambayo ina muhusu mwanafunzi(kama ilivyo pangwa na utawala Wa shule)
- Usalama barabarani (kama ilivyo pangwa na utawala wa shule)
- Safari za ki elimu (lazima mzazi na mwalimu mkuu wapitishhe)

Sababu zingine za kukosa shule huchukuliwa kuwa haramu.

### ***Je nahitaji kupiga simu shuleni kama mwanangu hatahuthuria shule ?***

Ndio.Wakati mwanafunzi atarudi shuleni lazima aje na barua kutoka kwa mzazi. Lazima barua iwe na tarehe ,sababu ya kutokua shuleni , na sahihi ya mzazi. Hii ni muhimu.

#### ***Mfano:***

Kwa yule yamuhusu ,  
John Smith hakuwa shuleni jumatatu ,tarehe moja mwezi wa tatu 2010, Kwa sababu alikuwa mgonjwa.  
Bi Smith.

Siku tatu (3) zikipita kama barua haijawafikia ofisi basi hiyo itakuwa ni haramu.

Kama mwanafunzi anazo siku tatu (3) hajahudhuria shule kiharamu basi wazazi wanaweza hitajika kulipa faini ya dola mia mbili (\$200).

### ***Je na kama mwanangu ana uteuzi na daktari wa meno au daktari?***

Kama ni lazima uteuzi ufanyike siku za shule , basi lazima barua ifikie shule SIKU MOJA KABLA ya uteuzi.

Pia, ukimpeleka mwanawe kwa daktari wa meno au daktari , tafathari waulize wakuandikie barua na upeleke ofisini wakati mwanafunzi atarejea shuleni. Kama mwanawe hatakuwa shuleni kwa muda mfupi wa uteuzi , lazima awe shuleni muda uliobakia.

### ***Je na kama mwanangu ni mgonjwa kwa muda mrefu ?***

Kama mwanawe amekosa shuleni siku tatu (3) au zaidi kwa sababu ya ugonjwa , tafathari muulize daktari wake akuandikie barua ya shule .Akikosa shule siku nyingi zaidi kwa sababu ya ugonjwa , unaweza ukaulizwa kuleta barua shuleni kila wakati mwanafunzi hajahudhuria.

## Taarifa otomatiki za simu na barua pepe

Katika usajili ,ulikamilisha umbo la taarifa otomatiki za simu na barua pepe ambazo hutumika kwenye mfumo wa Wilaya ya shule.kupitia mfumo huo , Wilaya inaweza kuwasiliana na wazazi kwa simu, barua pepe, na ujumbe mfupi Kuhusu kufungwa / kucheleweshwa kwa shule , tukio shuleni ,masuala muhimu ,na hali za dharura.

Tafathari mwambie katibu wa shule kama namba yako ya simu imebadilika wakati wa mwaka wa shule.

## Simu za mkononi

SHULE ZA MSINGI – Wanafunzi wanaweza kuja na simu ikiwa wameruhusiwa na mkuu wa shule.

SHULE ZA SEKONDARI - Wanafunzi wanaweza tumia simu za mkononi mwalimu akiwaruhusu.

## Mabadiliko ya Habari

Ni muhimu sana kuambia shule (kwa simu, barua pepe, ama barua ) kama namba ya mahali unapoishi au ya simu imebadilika.

## Siku za mzunguko

Mzunguko ni wa siku sita kulingana na ratiba yetu. Baada ya siku sita za shule , mzunguko unarudi siku ya kwanza.

### *Sampuli hapo chini*

Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa
Siku 1	Siku 2	Siku 3	Siku 4	Siku 5
Siku 6	Siku 1	Siku 2	Siku 3	Siku 4
Siku 5	Siku 6	Siku 1	Siku 2	Siku 3

## Nidhamu

Wanafunzi wana baadhi ya wajibu: Kuja shuleni kila siku ,Jitahidi darasani , na ufuatae kanuni za shule .Hakuna mwanafunzi anastahili kuingilia kati mchakato wa masomo ya mwingine. Wanafunzi wanatarajiwa kuheshimiana shuleni.Hatua ya nidhamu itachukuliwa kwa wanafunzi wasio na tabia nzuri.

## Kuondosha

### *Naweza fanya nini kama ningependa kuchukua mwanangu kutoka shule?*

Kama una mpango wa kumchukua mwanafunzi wako katika mwisho wa siku , Tafathari patiana barua siku hiyo. Utahitaji kuweka ishara kwa karatasi huko shuleni ili kumchukua mwanafunzi wako. Kama una mpango wa kuchukua mtoto wako KILA SIKU baada ya shule ,uta andika barua moja inayo elezea kwamba utamchukua kila siku . unaweza ulizwa uonyeshe kitambulisho .

Wanafunzi wa Shule za Sekondari hawahitaji barua kutoka kwa mzazi. Tafathari wasiliana na mwanafunzi wako kuhusiana na mipango ya kumchukua shuleni.

## **Mavazi na mapambo**

Wanafunzi wa Wilaya ya West Shore hawa vai sare za shule.

Wanafunzi wana wajibu wa kuweka mikono ,nywele ,na mavazi yao safi.

Kwenye darasa za masomo ya teknolojia ,sayansi ,familia na matumizi ya sayansi , na Elimu ya viungo ,wanafunzi walio na nywele ndefu wata hitajika kufunga nyuma kwa Usalama wao.

Mavazi ya kuonyesha mwili ,picha haifai ,ishara au maneno machafu ,kutumia madawa Ya kulevya ,pombe ,tumbako ,silaha ,au kushiriki ngono haikubaliki kamwe.

Wanafunzi hawakubaliwi kuvaa mavazi yaliyo raruka ,yanayo bana mwili au yanayo Chora mwili ulivyo. Nguo za ndani au chupi hazikubaliwi kuonyesha .

Mavazi kama vipuli , pete ,bangili ,mkufu yanayoweza kusababisha hatari kwa wanafunzi Hayataruhusiwa shuleni.

Kofia ,bendi na vitambaa za kichwa ( isipokuwa kwa sababu ya dini ) hazikubaliwi wakati Wa saa za Shule .

Lazima mashati yafunike tumbo . Ili mradi wanafunzi wavalie mavazi ya mkono mfupi , Nguo za ndani lazima zifunikwe .

.

Lazima kaptura na sketi ziwe na urefu wa katikati ya paja au zaidi.

Lazima wanafunzi wawe na viatu vizuri na salama.

## **Ufahamu wa dawa**

Dawa za kulevya na vifaa vya dawahaziruhusiwi kwa shule wakati wowote.Wanafunzi ambao hawatafuata kanuni hii ,watafukuzwa mara hio hio kutoka shuleni.

Kama mwanafunzi anahitaji dawa wakati shule inaendelea ,wazazi lazima wawasiliane na muuguzi wa shule .Agizo na ombi la dawa lazima lijazwe shuleni kabla ya dawa kupelekwa masaa ya shule.

Lazima mzazi (SIO mtoto ) apeleke shuleni dawa zote ambazo zitatumika wakati wa shule.

## **Safari ya Elimu**

***Ningependa kuenda na mwanangu safarini wakati wa shule.Je nifanye nini?***

Unastahili kujaza barua ya safari ya elimu siku tano (5 ) kabla ya safari. Mwanafunzi hakubaliwi kukosa shuleni zaidi ya siku tano (5) . Mwanafunzi hakubaliwi kukosa shuleni siku tano (5) za kwanza au siku kumi (10) za mwisho wa mwaka wa shule. Mwanafunzi haja ruhusiwa kukosa shuleni wakati wa mitihani ya katikati /fainali za mwisho wa mwaka.

***Je na kama nataka kurudi nchini kwetu kwa wiki kadhaa?***

Tafathari jadiliana haya na Mwalimu Mkuu.



## Huduma ya Chakula

*Tafadhali kumbuka: Katika mwaka wa masomo wa 2021-2022, kifungua kinywa na chakula cha mchana vitatolewa kwa wanafunzi wote bila gharama yoyote.*

*Mwanangu atanunua vipi kiamsha kinywa /chakula cha mchana shuleni ?*

Shule zote za Wilaya hutumia mfumo wa malipo ya mapema kwa kiamsha kinywa na chakula cha mchana kwa wanafunzi. Unaweza weka fedha kwenye benki ya K12paymentcenter.com (K12kituochamalipo.com) .Unaweza kuongeza pesa kwenye akaunti ya mwanafunzi kwa kutuma pesa au kulipa ukitumia cheti/hundi ya “mkahawa wa West Shore” kwenye bahasha ikiwa na jina la mwanafunzi ,namba ya kitambulisho cha shule na kiasi cha pesa mbele ya bahasha lile.

Wakati wa chakula cha mchana ,huenda pesa hazitakubalika .Lazima upatiane mwanzoni mwa siku.

## Chakula cha bure/ kilicho punguzwa bei

*Je mwanangu aweza kupata chakula cha bure au kilicho punguzwa bei?*

Kuna uwezekano. Tafadhali jaza ombi kutoka shule na urudidisha shuleni .Ombi moja tu lahitajika kutoka kwa kila familia .

Tafadhali taja majina ya watoto wako wote kwenye ombi.

**OMBI MPYA LAZIMA LIJAZWE KILA MWAKA.**

Ombi hilo huwa kwa lugha mingi tofauti .

## Unyanyasaji

Shule za Wilaya ya West Shore ni mahali salama kwa wanafunzi wote.Hakuna mwanafunzi atamtisha au kumnyanyasa mwenzake kwa kauli ya kudharau sababu ya rangi/taifa , kike/kiume,hali ya ndoa, mimba , au ulemavu. Kama mwanafunzi wako ameshuhudia matisho au ana nyanyaswa tafadhali mwambie Mwalimu Mkuu shuleni.

## Kazi ya ziada

Kazi ya ziada ni muhimu sana kwa mfumo wa shule hapa Marekani.

Madhumuni ya kazi hii ni kujifunza au kufanya mazoezi ya masomo uliyofunzwa darasani. Tafadhari uliza mwanao kuhusu kazi ya ziada na uhakikishe amekamilisha.

Kama huna uhakika wa vile inafanywa,tafadhali ongea na mwalimu.

## Kuchelewa

Je nitafanya nini kama mtoto wangu amechelewa kufika shuleni?

Tafadhali mpeleke mwanafunzi wako ofisini, na uandikishe sababu.

## Hifadhi

*Je kuna mahali pa kuhifadhi mali ya mwanafunzi? Shule ya msingi -Wanafunzi wanaweka mali yao darasani*

**SHULE YA SEKONDARI** - Wilaya imetenga mahali pa kuhifadhi kama vitabu,nguo ,nyenzo za shule ama vitu binafsi ambapo unaweza kupewa kwa kutuma maombi.

**HIFADHI SIO MALI YA MWANAFUNZI.**- Wafanya kazi wa shule wanaweza kuangalia ndani ya hifadhi wakati wowote.

## **Nyenzo/mali ya shule**

Je ni mali gani mwanangu anaweza peleka shuleni?

Shule huwapa wanafunzi wote vitabu vya kusoma.Katika shule za msingi ,wanafunzi huleta mfuko wa kuwekea vitabu ilhali shule za sekondari wanafunzi huleta mfuko wa vitabu ,folda,na kalamu.

Wanafunzi wa shule za msingi hawakubaliwi kubeba mifuko wakati wa shule lakini wa sekondari wanakubaliwa.

## **Mkutano wa mzazi-mwalimu**

*Mikutano kati ya mwalimu na mzazi ni ya kuongea kuhusu vile mwanafunzi anaendelea shuleni.*

Hizi mikutano hufanyika nyakati au msimu wa machipuko[spring] na msimu wa majani kuanguka [fall].Pia mzazi amekubaliwa kuwa na mkutano wakati wowote ako na swali.

## **Elimu ya viungo**

*Je kuna nguo maalum zimetengwa za darasa la mazoezi?*

Wanafunzi wa shule ya msingi sio lazima wavalie lakini lazima wavalie vitu vya raba. Shule za sekondari lazima wavalie hizo nguo maalum za mazoezi na viatu vya raba. Unaweza nunua hizo nguo shuleni au wavalie zao za nyumbani.

Tafadhali uliza mwalimu habari zaidi kuhusu elimu ya viungo.

## **Mtandao wa shule [PowerSchool]**

Wizara ya shule hutumia mtandao huu unaitwa powerschool.wazazi wanaweza tumia mtandao huu kuangalia vile mwanafunzi anaendelea shuleni kama matokeo ,mahudhurio ,na habari ya basi za shule.

Tafadhari wasiliana na shule ya mtoto wako kuweka ishara ili uweze kutumia huu mtandao.

## **Kanuni za basi ya shule**

1. Lazima uwe kwenye kituo cha basi dakika tano kabla ya basi kufika.
2. Kaa futi kumi nyuma mpaka basi lisimame na futi kumi mbali baada ya kutua kwenye basi.
3. Kama unavuka barabara ,vuka ukiwa mbele ya basi baada ya kuangalia kushoto na kulia .
4. Keti kwa kiti chako na angalia mbele.
5. Usisimame na usitoke kwenye kiti chako wakati basi linaenda.
6. Hakuna kupiga kelele au mayoye kwenye basi.
7. Hakuna kugonga wenzako au kurushwa vitu kwa basi.
8. Hakuna kukula ndani ya basi.



9. Mwili yako yote lazima iwe ndani ya basi,hakuna kuchungulia nje ya dirisha.
10. Usinguze mlango wa dharura.
11. Kuwa na heshima.
12. Sikiza dereva wa basi.
13. Usibebe chuma cha kuteleza au wanyama kwenye basi.
14. Usilete vyombo kubwa vya mziki au miradi kubwa kwenye basi .
15. Wilaya ya shule huchukua mkanda wa video kuona kinacho endelea kwenye basi ili kuhakikisha usalama barabarani.

Kama mwanafunzi hatafuata kanuni za basi,hataruhusiwa kutumia basi la shule.

## Saa za kuingia na kutokea shule

### Saa za kuingia saa za kutokea

Shule ya nasari [asubuhi]	8:45 a.m	-	11:30 a.m
Shule ya nasari [alasiri]	12:45 p.m	-	3:30 p.m
Shule ya msingi [darasa la Kwanza hadi tano]	8:45 a.m	-	3:30 p.m
Shule ya msingi [darasa la Sita hadi la nane]	7:38 a.m	-	2:45 p.m
Shule ya sekondari	7:37 a.m	-	2:45 p.m
Shule ya nasari iliyopita* [modified]	10:45 a.m	-	12:45 p.m

\*Hutumika wakati shule huchelewa masaa mawili asubuhi.shule ya nasari iliyopita haina athari kwa wanafunzi wa alasiri.

## Siku za kujifunza kwa njia ya masafa (remotely)

Kuna siku katika mwaka wa masomo ambazo wanafunzi watasoma kwa nusu siku wakiwa nyumbani. Kazi za wanafunzi zinaweza kukamilishwa katika siku ya kujifunza kwa njia ya masafa au wakati wowote katika mwisho wa wiki/likizo, na kuwasilishwa siku inayofuata ya masomo.

## Mipango ya michezo

*Je , kuna michezo inayofanyika shuleni?*

**SHULE YA MSINGI** - Hakuna michezo ya baada ya shule. Lakini kuna jumua ambazo zina michezo mbali mbali.

Wanafunzi wa darasa la saba na la nane wanaweza jiunga na michezo kama mpira wa miguu , soka , kukimbia , mchezo wa magongo kwenye shule ya sekondari. Mpira wa vikapu , wa wavu wa wasichana. Wanafunzi wanaweza pata habari zaidi kwa kuwasiliana na shule.

**SHULE YA SEKONDARI** - Kuna michezo mbali mbali na wanafunzi wanaweza pata habari zaidi kwa kuwasiliana na mwalimu wao.

## **Kujitolea**

### ***Naweza nikasaidia aje katika shule?***

Shule yakaribisha wazazi watakao jitolea kwenye shule na darasani. Kama ungetaka kujitolea ,uliza kwa habari zaidi.

## **Hali ya anga**

### ***Nini hufanyika kama hali ya anga imebadilika wakati wa shule?***

Kuna wakati shule itaanza kama imechelewa , watokee mapema , ama ifungwe.

### ***Kuchelewa shule masaa mawili asubuhi.***

Shule itaanza masaa mawili nyuma na saa za kawaida.

- Shule ya msingi itaanza saa 10:45 a.m
- Darasa la sita hadi la nane litaanza 9:38 a.m
- Shule ya sekondari itaanza 9:37 a.m

Kam mwanafunzi wako husafiri kwa basi kwenda shuleni , basi litawachukua masaa mawili nyuma .

Shule ya msingi hawana kiamsha kinywa siku ya kuchelewa shule. Darasa la sita hadi la nane la sekondari watapata kiamsha kinywa.

### ***Kutokea shule mapema***

Wanafunzi watatoka shule mapema kuliko saa za kawaida. Saa za kutoka hutengwa na wilaya.

### ***Kama kuna kuchelewa masaa mawili asubuhi , wanafunzi wa nasari wataenda shuleni?***

Wanafunzi wa nasari ya asubuhi wataenda saa 10:45 a.m hadi 12:45 p.m.

Wanafunzi wa nasari ya alasiri wataenda saa za kawaida.

### ***Habari ya kuchelewa shule , kutoka mapema , au kufungwa kwa shule nitaipata wapi ?***

Kuna njia nyingi ya kupata habari kama kuna mabadiliko yeyote.

- Sikiza simu otomaki kutoka wilaya ya West Shore.
- Angalia simu, barua pepe au ujumbe mfupi kutoka Wilaya ya West Shore.
- Angalia kurasa za Wilaya katika [www.wssd.k12.pa.us] , twita [@westshoreSD]
- Piga simu ya wilaya kuhusu hali ya anga kwa 938-3179.
- Angalia kwa runinga ya mitaa. Tafuta CUMBERLAND COUNTY-WEST SHORE SCHOOL DISTRICT ama YORK COUNTY-WEST SHORE SCHOOL DISTRICT, juu au chini ya runinga yako.

# BUILDING DIRECTORY

## Administration Center

Physical Address: 507 Fishing Creek Road,  
Lewisberry, PA 17339  
Phone: 717-938-9577  
Mailing Address: 507 Fishing Creek Road, P. O.  
Box 803, New Cumberland, PA 17070  
Twitter, Facebook, & Instagram @WestShoreSD

## HIGH SCHOOLS

### Cedar Cliff High School

1301 Carlisle Road, Camp Hill, PA 17011  
Phone: 717-737-8654  
Absence Calls: 717-920-0322  
Absence Emails: ccabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @CedarCliffColts  
Instagram @CedarCliff\_Colts

### Red Land High School

560 Fishing Creek Road, Lewisberry, PA 17339  
Phone: 717-938-6561  
Absence Calls: 717-938-6564  
Absence Emails: rlabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter and Instagram @RedLandHS

## MIDDLE SCHOOLS

### Allen Middle School

4225 Gettysburg Road, Camp Hill, PA 17011  
School & Absence Calls: 717-901-9552  
Absence Emails: alabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter and Instagram @AllenMustangs

### Crossroads Middle School

535 Fishing Creek Road, Lewisberry, PA 17339  
Phone: 717-932-1295  
Absence Calls: 717-938-3599  
Absence Emails: cmabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @CM\_Lightning  
Instagram @CMS\_Lightning

## New Cumberland Middle School

331 Eighth Street, New Cumberland, PA 17070  
School & Absence Calls: 717-774-0162  
Absence Emails: ncabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter and Instagram @NCMS\_Tigers

## ELEMENTARY SCHOOLS

### Fairview Elementary

480 Lewisberry Road, New Cumberland, PA 17070  
Phone: 717-774-2970  
Absence Calls: 717-901-9917  
Absence Emails: fvabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @FV\_Panthers

### Fishing Creek Elementary

510 Fishing Creek Road, Lewisberry, PA 17339  
Phone: 717-938-6565  
Absence Calls: 717-938-6567  
Absence Emails: fcabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @FCSharks1

### Highland Elementary

1325 Carlisle Road, Camp Hill, PA 17011  
Phone: 717-901-9860  
Absence Calls: 717-901-9715  
Absence Emails: hgabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @HG\_Stallions

### Hillside Elementary

516 Seventh Street, New Cumberland, PA 17070  
School & Absence Calls: 717-774-1321  
Absence Emails: hsabsent@wssd.k12.pa.us  
Twitter @HS\_Hedgehogs

### Newberry Elementary

2055 Old Trail Road, Eppers, PA 17319  
Phone: 717-938-2111  
Absence Calls: 717-938-9777  
Twitter @NB\_Bobcats

# BUILDING DIRECTORY

## **Red Mill Elementary**

700 Red Mill Road, Etters, PA 17319  
Phone: 717-938-3778  
Absence Calls: 717-938-3795  
Absence Emails: [rmabsent@wssd.k12.pa.us](mailto:rmabsent@wssd.k12.pa.us)  
Twitter and Instagram @RMDolphins

## **Rossmoyne Elementary**

1225 Rossmoyne Road, Mechanicsburg, PA 17055  
School & Absence Calls: 223-225-9729  
Absence Emails: [rsabsent@wssd.k12.pa.us](mailto:rsabsent@wssd.k12.pa.us)  
Twitter @RS\_bulldogs

## **Washington Heights Elementary**

531 Walnut Street, Lemoyne, PA 17043  
School & Absence Calls: 717-761-8040  
Absence Emails: [whabsent@wssd.k12.pa.us](mailto:whabsent@wssd.k12.pa.us)  
Twitter @WH\_Eagles

## ONLINE SCHOOL

### **ExCEL Virtual Learning Academy**

1225 Rossmoyne Road, Mechanicsburg, PA 17055  
School Calls: 223-225-9747  
Absence Emails: [dlabsent@wssd.k12.pa.us](mailto:dlabsent@wssd.k12.pa.us)  
Twitter and Instagram @ExCEL\_VLA





# West Shore SCHOOL DISTRICT

INSPIRE • ENGAGE • EMPOWER

## Our Pledge

We are committed to providing students with inspiring and relevant experiences so they may live meaningful, purposeful, and impactful lives.

## Board of School Directors

Brian K. Guistwhite, President  
Christopher J. Kambic, Vice President  
Judith A. Crocenzi  
Edward G. Fogel  
Frank J. Kambic  
Sheri D. Moyer  
Frederick A. Stoltenburg  
Heidi E. Thomas  
Abigail A. Tierney

## Non-Members

Ryan E. Argot, Ed.D., Secretary  
TBD, Treasurer  
Brooke E.D. Say, Esq., Solicitor

## Administration

Todd B. Stoltz, Ed.D., Superintendent  
Jamie A. Whye, Ed.D., Assistant Superintendent

The West Shore School District will provide to all persons equal access to all categories of employment in this District, regardless of race, age, color, creed, religion, sex, gender, gender identity, sexual orientation, ancestry, genetic information, marital status, pregnancy, national origin, handicap/disability, or differently-abled status, in accordance with state and federal laws governing educational and vocational programs and in its recruitment and employment practices. The District shall make reasonable accommodations for identified physical and mental impairments that constitute disabilities, consistent with the requirements of federal and state laws and regulations. Inquiries concerning the application of Title VII, Title IX, Section 504, the ADA, and the implementing regulations may be referred to the Director of Human Resources, 507 Fishing Creek Road, P.O. Box 803, New Cumberland, PA 17070-0803, telephone 717-938-9577.

UPDATED MAY 2021